**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MJI GEITA**

**Kumb. Na. AB.55/451/01/65** **TAREHE: 13/01/2023**

# YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Geita anawatangazia wananchi wote nafasi za ajira ya kudumu kwa kada ya Watendaji wa Mitaaa kama Ifuatavyo.

## 1.0 MTENDAJI WA MTAA DARAJA III - NAFASI MBILI (02)

### 1.1 MAJUKUMU YA KAZI.

- Kusimamia na kutekeleza sheria ndogo pamoja na sheria nyingine zinazotumika katika Mtaa.
- Kushauri kamati ya Mtaa kuhusu mipango ya maendeleo katika Mtaa.
- Kuratibu utekelezaji wa Sera na Sheria zinazotekelezwa na Halmashauri katika Mtaa.
- Kusimamia na kutekeleza mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umaskini katika Mtaa.
- Kusimamia ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote.

### 1.2 SIFA ZA MWOMBAJI:

i. Mwombaji awe na Elimu kidato cha Nne (IV) au sita (VI).
ii. Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
iii. Awe na Umri kuanzia miaka 18 hadi miaka 45.
iv. Awe ni raia wa Tanzania.

1.3 **MSHAHARA:**

Ngazi ya Mshahara ni **TGS B.**

**NB:** Mtumishi atakayeajiriwa hataruhusiwa kuhama kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu (3) tangu tarehe yake ya ajira.

**UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI**

Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **26/01/2023** saa **9:30** Alasiri. Maombi yatumwe kwa njia ya Posta kwa **S.L.P 384, Geita** au yaletwe Masjala ya Halmashauri ya Mji Geita, watakaokidhi vigezo watajulishwa kwa simu na katika mbao za matangazo ili kuweza kuja kwenye usaili.

Tangazo hili limetolewa na,

*Egidy Teulas,*

**KAIMU MKURUGENZI WA MJI.**

MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
GEITA.